

**ATHARI ZA KIKIKUYU KATIKA KUJIFUNZA LUGHA YA KISWAHILI SANIFU
KATIKA SHULE ZA UPILI, KAUNTI NDOGO YA OTHAYA, KAUNTI YA NYERI,
KENYA**

NA

VINCENT WANJALA

EDU-G-4-0851-19

EVANS OGINGA

EDU-G-4-0916-19

FREVIAN MWAURA

EDU-G-4-1001-19

**UTAFITI HUU ULIWASILISHWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA
MAHITAJI YA SHAHADA YA KWANZA KATIKA SHULE YA UALIMU, CHUO
KIKUU CHA GRE TSA, THIKA.**


NOVEMBA 2022

UNGAMO

Pendekezo hili la utafiti ni kazi yetu asilia na halijawasilishwa kutimiza mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu chochote.

Vincent Wanjala


EDU-G-4-0851-19

Sahihi 

Tarehe 06/12/2022

Evans Oginga


EDU-G-0916-19

Sahihi 

Tarehe 06/12/2022

Frevian Wanjiku


EDU-G-4-1001-19

Sahihi 

Tarehe 06/12/2022

Bw. Edwin Muna

MSIMAMIZI: Nathibitisha kwamba pendekezo hili lilitayarishwa na watahiniwa waliotajwa hapo juu, chini ya usimamizi wangu.

Sahihi 

Tarehe 06/12/2022

Shule ya Ualimu, Chuo Kikuu cha Greta

SHUKRANI

Watafiti wanamshukuru mwenyezi mungu kwa kuwapa uhai, maarifa na uwezo wa kufikiri wakati walikuwa wanaushughulikia utafiti huu

Shukrani zingine za dhadi nikwa msimamizi wetu Bw. Edwin Muna kwa maelekezo, ushauri na uvumilivu wake kwakutuongoza kutoka mwanzo hadi mwisho wa utafiti huu. Shukrani ziwafikie wazazi wetu kwa kutupa hela ambazo tulizitumia katika kufanikisha harakati hii nzima ya kutafitia lugha ya kikikuyu nyeri.

Wanafunzi walioshiriki, walimu wakuu wa shule za upili Othaya na walimu wa Kiswahili sanifu wapate shukrani za dhati kwa mchango wao mkubwa ambao ulifanya shughuli hii nzima kukamilika.

TABARUKU

Kwa Chama Cha Kiswahi Chuo Kikuu Cha Greta, Thika (CHAKIGRE)

Yaliyomo	
UNGAMO.....	i
SHUKRANI.....	ii
TABARUKU	iii
Akronimi na Vifupisho	vii
Fasili ya Istilahi Muhimu	viii
IKISIRI	ix
1.1 Usuli Wa Mada.....	1
1.2 Tatizo La Utafiti	3
1.4 Kiunzi Cha Dhana	3
1.3 Malengo Ya Utafiti.....	4
1.5 Maswali Ya Utafiti	5
1.7 Umuhimu Wa Utafiti.....	5
1.8 Upeo Wa Utafiti.....	5
1.9 Changamoto Katika Utafiti.....	6
2.1 Utangulizi	7
2.2 Yalioandikwa Kuhusu Athari Za L1 Katika Kujifunza L2	7
2.3 Yaliyoandikwa Kuhusuathari Za L1 Katika Upatanisho Sahihi Wa Kisarufi Katika Sentensi.....	8
2.4 Yalioandikwa Kuhusu Matumizi Yafaayo Ya Msamiati	9
2.5 Yalioandikwa Kuhusu Athari Za L1 Katika Utamkaji Ufao Wa Sauti	10
2.6 Msingi Wa Nadharia.....	13
Nadharia Ya Uchanganuzi Makosa (UM).....	13
2.7 Mapengo Ya Utafiti	14
SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI	15
Utangulizi	15

3.1 Mbinu Za Utafiti	15
3.2 Eneo La Utafiti	15
3.3 Idadi Ya Walengwa	15
3.4 Uteuzi Wa Sampuli.....	15
Vifaa Vya Utafiti	16
Utafiti Huu Utatumia Vifaa Vifuatavyo:	16
3.6 Mbinu Za Ukusanyaji Wa Data	16
3.7 Mbinu Ya Uchanganuzi Wa Data.....	17
3.8 Maadili Ya Kuzingatiwa Katika Utafiti.....	17
3.9 Uhalali Wa Utafiti	17
SURA YA NNE: MATOKEO NA MAJADILIANO	18
4.2 Kiwango Cha Upokezi Wa Majibu Ya Wahojiwa	18
4.3 Uchanganuzi Wa Data.....	18
4.4 Upatanisho Sahihi Wa Kisarufi.....	19
4.5 Matumizi Yafaayo Ya Msamiati	20
4.5.1 Ubadilishaji Fonimu	20
4.6 Utamkaji Ufaao Wa Sauti Za Kiswahili.....	21
4.6.1 Udondoshaji.....	22
4.6.2 Uchopekaji.....	23
SURA YA TANO: MHUTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO	24
5.0 Utangulizi	24
5.1 Mhutasari wa utafiti	24
5.1.1 Upatanisho sahihi wa kisarufi.....	24
5.1.2 Matumizi Yafaayo Ya Msamiati	24
5.1.3 Utamkaji Ufaao Wa Sauti Za Kiswahili Sanifu.....	24

5.2 Hitimisho Ya Utafiti.....	25
5.3 Mapendekezo Ya Utafiti	25
5.4 Mapendekezo Zaidi	26
MAREJELEO	27
VIAMBATISHO.....	30
Kiambatisho I: Barua ya Ombi la Kukusanya Data	30
Uandishi wa insha kwa wanafunzi	31

Akronimi na Vifupisho

L1: lugha ya kwanza

L2: Lugha ya pili

BAKITA: Baraza la Kiswahili Tanzania

UM: Uchanganuzi Makosa

KNEC: Baraza la Mitihani Nchini Kenya

Fasili ya Istilahi Muhimu

Lugha ya kwanza: lugha ambayo mtu hujifunza kabla ya kujifunza lugha yoyote ile

Lugha ya pili: lugha ambayo binadamu hujifunza baada ya kujifunza ile ya kwanza

Wazungumzaji: wazungumzaji wazawa wa Kikikuyu

IKISIRI

Watu wengi hukumbwa na matatizo kadha wanapojifundisha na wanapofundishwa lugha fulani hasa lugha ya pili katika Maisha yao. Matatizo haya husababisha changamoto katika maisha ya mhusika ikiwemo mawasiliano na elimu. Lengo kuu la utafiti huuni kubaini athari za lugha ya kikikuyu katika kujifunza lugha ya Kiswahili katika kaunti ndogo ya Othaya, kaunti ya Nyeri. Malengo ya utafiti huu ni; Kubaini namna kikikuyu kinavyoathiri uwezo wa wanafunzi wa kutumia upatanisho sahihi wa kisarufi katika sentensi katika shule za upili, kaunti ndogo ya Othaya, Nyeri Nchini Kenya, Kuweka wazi athari za kikikuyu kwa uwezo wa wanafunzi wa matumizi yafaayo ya msamiati katika shule za upili, kaunti ndogo ya Othaya, kaunti ya Nyeri, Nchini Kenya, Kubaini namna kikikuyu kinaathiri uwezo wa wanafunzi wa utamkaji ufaao wa sauti katika shule za upili, kaunti ndogo ya Othaya, kaunti ya Nyeri, nchini Kenya. Utafiti ulilenga jumla ya shule 34 zilizo na jumla ya wahojiwa 14,314. Mbinu za uteuzi wa sampuli wa mpangilio na uteuzi wa maksudi. Mbinu za ushiriki na insha zilitumiwa katika kukusanya data. Data zilichanganuliwa kwa kutumia mfumo wa tarakilishi wa kuchanganua data za kisayansi wa SPSS. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba lugha ya Kikuyu inaathiri uwezo wa wanafunzi kutumia upatanisho sahihi wa kisarufi, pia ilibainika kuwa wanafunzi waliokuwa wameathiriwa na lugha hii wanashindwa kutumia misamiati ya Kiswahili vilivyo. Zaidi, utafiti ulionyesha kuwa lugha ya kikuyu huathiri wazungumzaji wanafunzi wayo katika utamkaji wa sauti za Kiswahili sanifu.

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

Sura hii ilianguzia usuli wa mada, tatizo la utafiti malengo ya utafiti, maswali yautafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete katika utafiti, kiunzi cha dhana, changamoto zautafiti, machukulio ya utafiti na upeo wa utafiti.

1.1 Usuli Wa Mada

Lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya lugha zinazofundishwa kama lugha ya pili nchini Kenya. Kujifunza lugha ya pili huweza kuathiriwa na lugha ya kwanza na katika mkutadha huu ni lugha ya kikikuyu. Tafiti za awali kama ile ya Masasa (2017), kuhusu athari ya matamshi ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili, Alitumia nadharia ya Selinker (1972) ya kuhusisha wanaojifunza lugha katika maandishi na kuzungumza. Anabaini kuwa, lugha ya kwanza huathiri kujifunza lugha ya Kiswahili.

Utafiti mwingine wa awali uliofanywa na Alonso (2016) katika Chuo Kikuu cha Vigo kuhusu athari ya lugha ya kwanza kwa ujifunzaji na mapokezi ya lugha ya pili. Alitumia nadharia ya kufikiri ndani ya kufikiri kwa kuongea (Bylund et al (2013). *The 'thinking in thinking for speaking, language interaction and acquisition'*) ya Athanasopouly P. na Bylund (2013). Katika utafiti huu R. Alonso anasema kwamba lugha ya kwanza huathiri hali ya mtu ya kufikiri na hili hufanyika moja kwa moja bila kufunzwa na yeyote. Utafiti huu ulibaini kwamba lugha ya kwanza humwathiri binadamu anapojifunza lugha ya pili.

Nchini Brazil, Kireno ndiyo lugha ya taifa na hufunzwa katika shule nchini humo kama lugha ya pili kwani ndio nchi pekee kutawaliwa na wareno Amerika kusini na kurithi lugha ya Kireno kama lugha rasmi. Brazil ina Zaidi ya lugha mia moja themanini asilia zinazozungumzwa nchini humo. Kulingana na shirika la Alphatrad, Kiwango cha Brazil cha kusomanakuandika Kireno ni themanini na sita nukta nne (86.4) ambacho nicha chini Zaidi ya nchi zote za Amerika kusini. Hii ni wazi kwamba lugha za kwanza ambazo huzungumzwa nchini humo na wenyeji zina athari kwa kujifunza lugha ya kireno ambao ndio lugha ya pili.

Nchini Ugiriki, Kigiriki ndio lugha ya wenyeji na ambayo huzungumzwa na watu wengi nchini humo. Lugha ya pili Nchini humo ni kiingereza ambayo hutumika katika shughuli za kibiashara na pia hutumika katika kutoa mafunzo katika taasisi nyingi za kielimu. Kulingana na takwimu nchini humo, lugha ya kigiriki bado inatumika kwa mapana na asilimia tisaini na tisa nukta tano

(99.5%) huzungumzwa nchini humo. Hii ni wazi kwamba kigiriki ni lugha asilia na pia ni lugha ya kufunzia na hivyo asilimia kubwa wakaazi ni wamilisi wa lugha hiyo kama lugha asilia.

Nchini Tanzania, asilimia kubwa ya wakazi wake huzungumza lugha ya Kiswahili kama lugha ya kwanza. Lugha ya Kiswahili pia hutumiwa kufunzia masomo mengi nchini humo. Takwimu zinaonyesha kwamba asilimia kubwa ya Watanzania huzungumza lugha ya Kiswahili kwa ufasaha kwani wao hukizungumza Kiswahili kama lugha yao ya kwanza na wengi. Utafiti wa shirika la lugha na utamaduni Tanzania (2015) lilibainisha kwamba kati ya watu saba, watano kati yao huzungumza Kiswahili kama lugha asili ya kwanza kando na lugha yao asili. Hii ni kwa sababu wao hujifunza lugha ya Kiswahili pinde tu wanapozaliwa na kuanza kujifunza kuzungumza.

Nchini Kenya, kila jamii ina lugha yake asilia, kulingana na takwimu za hivi karibuni, kuna makabila arubaini na saba na kila kabila lina lugha yake. Lugha ya Kiswahili na Kiingereza ndizo lugha rasmi za mawasiliano na ndizo lugha ambazo hufunzwa shuleni kama lugha ya pili.

Lugha ina nafasi muhimu sana katika uzalishaji wa maarifa nakuleta tofauti zililopo kati ya binadamu na viumbe wengine. *Barasa* (2005) anaeleza kwamba watu hupata maarifa ya lugha, kuelewa jinsi ya kuweka maarifa haya kwa mifumo ambayo binadamu husoma na kumiliki. Usomaji wa Kiswahili kama lugha ya pili imekumbwa na matatizo mengi kuanzia enzi za ukoloni hadi sasa.

Athari ya lugha ya kwanza katika kujifunza lugha ya Kiswahili ni tatizo linalokabili binadamu wengi wanapokuwa wanajifunza kuongea lugha ya pili ambayo kwa muktadha huu ni lugha ya Kiswahili na Kiingereza. *Masasa* (2017) anaeleza kwamba, Binadamu anapoanza kujifunza lugha ya pili atakumbana na matatizo mbalimbali kama vile matamshi, lafudhi na mkazo wa maneno. Tatizo hili linatokana na lugha mama ambayo ni lugha ya kwanza ya mzungumzaji wa Kiswahili. Mzungumzaji anakuwa na umilisi katika lugha ya kwanza ndiyo maana anapata shida pale anapongea lugha ya pili kwani matamshi, lafudhi vinakuwa vimezoeleka katika lugha ya kwanza na hivyo kumuia vigumu kubadilika katika lugha ya pili ambayo ni lugha ya Kiswahili.

Otiende (2013) anasema kuwa swala la athari ya kujifunza lugha ya pili kuna tofauti za kifonolojia kati ya lugha hizo mbili ambazo huathiri matumizi ya lugha ya pili miongoni mwa

wakaazi. Anaendelea kwa kusema kwamba baadhi ya fonimu hutofautiana katika matumizi kati ya lugha asili na lugha ya pili.

Jamii ya wakikikuyu inapatikana eneo la kati ya Kenya. Katika utafiti huu, watafiti waliangazia athari za Kikikuyu kwa kujifunza Kiswahili katika kaunti ndogo ya Othayo, kaunti ya Nyeri nchini Kenya. Hili ni eneo ambalo wakazi wengi huzungumza lugha ya kikikuyu kama lugha yao ya kwanza. Eneo hili lina shule tofauti ambapo kuna shule za mabweni ambazo huwasajili wanafunzi kutoka maeneo mengine na ambao huwa na lugha za kwanza tofauti. Watafiti waliangazia kubaini ikiwa matokeo ya somo la Kiswahili. Kutokana na hizi athari, pana haja ya kufanya utafiti huu ili kubaini kama athari hizi za Kikikuyu ndizo zinachangia matokeo haya.

1.2 Tatizo La Utafiti


Watafiti walichunguza athari za lugha ya kikikuyu katika kujifunza Kiswahili katika shule za upili kaunti ndogo ya Othaya. Watafiti walifafanua matatizo anayokumbana nayo mwanafunzi wa kikikuyu katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wengi kaunti ndogo ya Othaya huzungumza lugha ya kikikuyu kama lugha yao ya kwanza na watafiti walifafanua matatizo anayokumbana nayo mwanafunzi wa kikikuyu wakati anapotunga sentensi za Kiswahili, anapotamka maneno ya Kiswahili na ni jinsi gani anatumia msamiati wa Kiswahili.

Wanafunzi wengi wa asili ya kikikuyu waliosoma na wanaosomalugha ya Kiswahili hukumbwa na athari za lugha ya kikikuyu wanapotunga sentensi za Kiswahili. Vilevile wanafunzi hawa hukumbwa na athari za kimatamshi, matumizi yafaayo ya maneno katika mikitadha tofauti. Kutokana na changamoto hizi watafiti waliona umuhimu wa kutafitia na kujua athari hizo ni vipi.

1.4 Kiunzi Cha Dhana

K.H

K.T



1.3 Malengo Ya Utafiti

1.3.1 Lengo Kuu La Utafiti Kubaini athari za Kikikuyu katika kujifunza Kiswahili sanifu katika shule za upili, Kaunti Ndogo ya Othaya, Kaunti ya Nyeri, nchini Kenya.

1.3.2 Malengo Mahususi Ya Utafiti.

- i) Kubaini namna Kikikuyu kinavyoathiri uwezo wa wanafunzi wa kutumia upatanisho sahihi wa kisarufi katika sentensi katika shule za upili, Kaunti Ndogo ya Othaya, Nyeri, nchini Kenya.
- ii) Kuweka wazi athari za Kikikuyu kwa uwezo wa wanafunzi wa matumizi yafaayo ya msamiati katika shule za upili, Kaunti Ndogo ya Othaya, kaunti ya Nyeri, nchini Kenya.
- iii) Kutambua namna Kikikuyukinavyoathiri uwezo wa wanafunzi wa utamkaji ufaao wa sauti za Kiswahili sanifu katika shule za upili, Kaunti Ndogo ya Othaya, Kaunti ya Nyeri, nchini Kenya.

1.5 Maswali Ya Utafiti

1. Kikikuyu kinaathiri vipi uwezo wa mwanafunzi kutumia upatanisho sahihi wa kisarufi katika sentensi katika shule za upili, kaunti ndogo ya Othaya, kaunti ya Nyeri, Nchini Kenya?
2. Kikikuyukinaathiri vipi uwezo wa mwanafunzi wa matumizi yafaayo ya msamiati wa Kiswahili sanifu katika shule za upili, kaunti ndogo ya Othaya, kaunti ya Nyeri, Kenya?
3. Je, Kikikuyu kinaathiri vipi uwezo wa mwanafunzi wa utamkaji ufaao wa sauti za Kiswahili sanifu katika shule za upili, Kaunti Ndogo ya Othaya, Kaunti ya Nyeri, Kenya?

1.6 Nadharia Tete Za Utafiti

H_0 Kikikuyukinaathiri uwezo wa wanafunzi wa kutumia upatanisho sahihi wa kisarufi katika sentensi katika shule za upili, Kaunti Ndogo ya Othaya, Nyeri, nchini Kenya.

H_1 : Kikikuyu kinaathiri uwezo wa wanafunzi wa kutumia msamiati ufaao katika shule za upili, Kaunti Ndogo ya Othaya, Kaunti ya Nyeri, nchini Kenya.

H_2 : Kikikuyu kinaathiri uwezo wa wanafunzi wa utamkaji ufaao wa sauti za Kiswahili sanifu katika shule za upili, Kaunti Ndogo ya Othaya, Kaunti ya Nyeri, nchini Kenya.

1.7 Umuhimu Wa Utafiti

Utafiti huu ni wa muhimu kwa sababu zifuatazo:

Matokeo ya utafiti huu yatawasaidia wanafunzi wa shule za upili Kaunti Ndogo ya Othaya kutambua athari za Kikikuyu katika kujifunza kwao Kiswahili sanifu ili wajikakamue kuondosha athari hizo. Vilevile, matokeo ya utafiti huu yatawasaidia walimu wa somo la Kiswahili wa Kaunti Ndogo ya Othaya, Kaunti ya Nyeri, nchini Kenya kutambua athari za Kikikuyu kwa ufunzaji Kiswahili sanifu kwa wanafunzi wao. Ufahamu huo utawafaa katika kuweka mikakati ya kabili athari zitakazotambuliwa.

1.8 Upeo Wa Utafiti

Watafiti wanachunguza athari za Kikikuyu katikakujifunza lugha ya Kiswahili sanifu katika kaunti ndogo ya Othaya. Utafiti unashughulikia athari za kiisimu katika ujifunzaji wa Kiswahili, upatanisho ufaao wa kisarufi, Matumizi yafaayo ya msamiati na utamkaji ufaao wa sauti za Kiswahili. Utafiti huu unalenga takriban shule kumi za kutwa na shule kumi zingine za bwani.

1.9 Changamoto Katika Utafiti

Utafiti huu utahusisha wanafunzi na walimu wa kiswahili katika kaunti ndogo ya Othaya. Watafiti wanaweza kukumbwa na changamoto zifuatazo:

Huenda wanafunzi fulani wakaandika insha zao kwa maandishi yasiyosomeka kwa urahisi na watafiti. Hata hivyo, watafiti watahakikisha kuwa wanapitia kila insha kabla ya kutmatisha shughuli za ukusanyaji data ili kuhakikisha kuwa kila mojawapo inasomeka vyema. Baadhi ya hojaji watakazopewa vyanzo huenda zisijazwe ipasavyo na nyingine kukosa kurejeshwa. Watafiti watahakikisha kuwa kila hojaji imejazwa kikamilifu kabla ya kuzipokea kutoka kwa vyanzo. Vilevile, watafiti watawapa vyanzo hojaji na kuwaomba kuzijaza katika kikao kimoja ili kuhakikisha kila mojawapo inajazwa kikamilifu na kurejeshwa.

SURA YA PILI: YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

2.1 Utangulizi

Katika sura hii, Watafiti waliangazia kazi zilizoandikwa awali kuhusu; athari za L1 katika kujifunza L2, athari ya L1 kwa matumizi ya msamiati ufaao, upatanisho sahihi wa kisarufi katika sentensi na utamkaji ufaao wa sauti, msingi wa nadharia katika utafiti huu na pengo la utafiti.

2.2 Yalioandikwa Kuhusu Athari Za L1 Katika Kujifunza L2

Lugha ya kwanza huwa na athari kubwa katika kujifunza lugha ya pili, Kulingana na Masasa(2017) akimnukuu Corder (1967) yeye (Corder) katika utafiti wake kuhusu nadharia ya lugha kadirifu na uchanganuzi makosa anasema kwamba uchanganuzi wa makosa ni muhimu sana kwa kuwa huwawezesha watafiti kujua namna watu hujifunza lugha na michakato wanayotumia katika harakati za kutambua lugha lengwa. Wanaojifunza hukiuka kaida za L2. Wanafunzi wa L2 mara nyingi huhamisha usemi wa L1 na kutumia sheria zake katika L2 anaendelea kusema kwamba matatizo yanayojitokeza mtu anapojifunza L2 ni swala la kawaida kutokea. Kabla ya Mwanafunzi kuzoea matumizi kamili ya kanuni ya L2 hufanya makosa mengi ya kiisimu. Corder (1967) anafautisha makosa na matatizo yanayokumbana nayo mwanafunzi anapojifunza L2. Kulingana naye, makosa ni matatizo yanayotokana na utendaji na hayana kikwazo chochote na yanaweza kutokea katika hali zozote. Hata hivyo makosa yanadhihirika kwa kuzingatia umilisi na utendaji wa lugha. Kazi hii ilisaidia katika utafiti wa athari za kikikuyu katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Ingawa utafiti wa Masasa unazungumzia athari za kijita katika kujifunza Kiswahili sanifu, utafiti huo haujaonesha athari za kikikuyu katika kujifunza lugha ya Kiswahili kama L2.

Masasa (2017) akiwanukuu Gass na Selinker (1994) anasema kwamba makosa yanayofanywa na wanafunzi wanapojifunza L2 kama ishara wazi zilizodhihirisha ujuzi wa mwanafunzi katika L2. Makosa haya hutumiwa na watafiti katika juhudi zao za kugundua mikakati inayotumiwa na watu katika upataji wa L2. Makosa yalianza kuchukuliwa kama elementi za utafiti wa kiisimu ambazo zilikuwa zimepuuzwa kwa kipindi kirefu. Aidha, makosa yalionekana kama mifumo ya kiisimu ambayo ilitumiwa na wanafunzi katika mawasiliano na ujifunzaji wa lugha lengwa.

Ontieri (2014) akimnukuu Richards (1974), anasema kwamba tajriba ya mwanafunzi katika L1 huhamishwa katika L2 kwa lengo la kurahisisha ujifunzaji wa lugha hiyo. Uhamishaji wa aina

hii husababisha kuwapo kwa makosa mbalimbali hususani iwapo mifumo ya lugha mbili husika ni tofauti. Hata hivyo, kupitia kwa makala haya tunathibitisha kuwa athari za kifonolojia hazidhihiriki katika lugha zenye mifumo tofauti pekee bali hata zile ambazo zina mifumo inayofanana. Upekee katika lugha mbalimbali, hata kama ni za kundi moja, husababisha athari ambazo zinaweza kuwekwa bayana kwa uchanganuzi makini wa viwango tofauti vya kiisimu. Makala hii inaweka wazi athari za kifonolojia kutokana na lugha ya Kikamba na Kikisii. Kiswahili tukizingatia michakato mitatu: udondoshaji na uchopekaji. Mifano inayoonesha athari za kifonolojia imetokana na utafiti wa uwandani (Ontieri, 2010) uliofanywa katika wilaya ya Nakuru nchini Kenya ambapo wanafunzi mia moja waliandika insha ambazo zilichanganuliwa.

Hata hivyo tafiti hizi hazijaangazia athari za kikikuyu katika kujifunza Kiswahili kaunti ndogo ya Othaya.

2.3 Yaliyoandikwa Kuhusuathari Za L1 Katika Upatanisho Sahihi Wa Kisarufi Katika Sentensi.

Upatanisho wa kisarufi ni muundo wa maneno ukizingatia ngeli ya nomino inayotumika. Kwa mujibu wa BAKITA (2015), upatanisho wa kisarufi ni kukubaliana kisarufi kunakojitokeza kati ya nomino, kiima na kitenzi au na kivumishi kunakobainishwa na viambishi.

Obara (2014) akimnukuu Rapando (2005) anasema kwamba katika utafiti wake alipochunguza makosa ya kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika uandishi wa insha jijini Nairobi. Katika utafiti huu Rapando aligundua kuwa, baadhi ya makosa ya wanafunzi yanasababishwa na lugha ya kwanza, kiingereza na lugha ibuka ya Sheng. Utafiti huu ulisaidia katika utafiti huu wa athari ya lugha ya Kikikuyu katika kujifunza lugha ya kiswahili. Ingawa utafiti wa Rapando (2005) ulizungumzia athari za kujifunza lugha ya kwanza hadi lugha ya pili bado utafiti huo haujaonyesha athari katika lugha ya Kikikuyu. Hilo ndilo pengo ambalo utafiti huu ulishughulikia.

Kisakwah (2014) katika Tasnifu yake kwa hitaji la shahada ya Uzamili katika Chuo kikuu cha Nairobi ambapo alifanya Utafiti kuhusu uchanganuzi makosa na muundo wa sentensi za Kiswahili. Ulinganisho wa Sentensi sahili za Kiswahili sanifu na za Kisuba. Katika Utafiti huo ilibainika kuwa kuna makosa mengi katika insha walizoandika wanafunzi wa kisuba. Makosa haya yalibusu vipashio vyote vya Kiisimu. Mtafiti huyo aliangalia athari zilizoletwa na makosa

yaliyokana na athari ya Lugha ya kwanza (L1). Lakini bado utafiti huu haujazungumzia athari za L1 katika upatanisho sahihi wa kisarufi. Kwa hali hiyo utafiti huu ulisaidia pengo hili la Kikikuyu katika kujifunza lugha ya Kiswahili Sanifu.

Curtain (1990) akinukuliwa na Nambula (2011), katika utafiti wake uliohusu wanafunzi wanaojifunza L2, anasema kwamba ni vyemawanafunzi kuelewa miundo na misingi ya lugha hiyo na pia matamshi bora wanapojifunza. Uhusiano uliopo kati ya lugha mbili ni muhimu kwa kuwa lugha huathiriana wakati binadamu anajifunza lugha yoyote ile. Aidha wameongezea kuwa, L1 huathiri ujifuzaji wa L2 kwa binadamu. Kazi ya mwandishi huyu ilifaa sana katika utafiti huu kwa kuwa kazi yao ilitilia mkazo suala la mwingiliano baina ya lugha mbili na pia kwa kuangazia athari ya lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Kwa hiyo kazi yao imeniwezesha kuangalia athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya kiswahili hivyo, ulinganisho wa sentensi za lugha hizo umechangia pakubwa katika kubaini athari ya lugha ya kijita katika kujifunza lugha ya kiswahili. Vile vile, kazi hiyo ilikuwa data toshelezi ya kudondoa maneno yenye athari ya lugha ya kwanza na kisha kuzioanisha ili kupata tofauti zinazojitokeza kati ya lugha hizo mbili. Ingawa utafiti wa Curtain (1990) unazungumzia athari za lugha katika kujifunza lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili bado utafiti huo haujaonesha athari katika lugha ya Kikikuyu. Hivyo ndilo pengo ambalo utafiti huu ulishughulika nalo.

2.4 Yalioandikwa Kuhusu Matumizi Yafaayo Ya Msamiati

Obara (2014), alifanya utafiti kuhusu uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na Wanafunzi wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii. Katika utafiti wake, ilijitokeza kuwa makosa yanayojitokeza katika Insha za Wanafunzi hutokea katika Viwango vyote vya Usomi. Makosa haya huendelea kupungua kadri Mwanafunzi anavyoendelea katika viwango vya Juu vya usomi. Katika utafiti huo ilibainika wazi kuwa Wanafunzi hufanya makosa haya kwa sababu ya kuhamisha mifumo ya kiisimu ya L1 hadi L2. Ilibainika kwamba Lugha ya Ekegusii haina fonimu /l/ na kwa hivyo Mwanafunzi anapoandika neno kama /leta/ hutumia fonimu inayopatikana katika Lugha yake ya kwanza hivyo ataandika /reta/ badala ya /leta/. Makosa haya yamekiuka kanuni za kifonolojia za Kiswahili Sanifu. Lakini ikumbukwe kuwa makosa hayawi kizuizi cha ujifunzaji Lsugha ni harakati za Mtu kuimudu L2. Hivyo utafiti huo umebaini chanzo cha matokea mabaya katika Somo la Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii. Utafiti huu umeangalia L1 Ekegusii na lugha ya pili ya Kiswahili lakini bado

haujazungumzia kwa upande wa lugha ya Kikikuyu katika matumizi yafaayo ya msamiati wa kiswahili. Hivyo lengo hilo ndilo watafitiwalishughulika nalo.

2.5 Yalioandikwa Kuhusu Athari Za L1 Katika Utamkaji Ufaao Wa Sauti

Kulingana na utafiti uliofanywa na Ontieri kuhusu athari za kifonolojia za lugha ya kwanza katika kiswahili: mfano wa lugha teule za kibantu nchini Kenya (2010) anasema kwamba,

“Athari za kifonolojia hujitokeza katika mazingira ambapo lugha moja huiathiri nyingine hasa ikiwa mifumo ya uundaji silabi ni tofauti. Hali hii huonekana kupitia kwa uhamishaji wa mifumo ya kifonolojia kutoka lugha ya kwanza hadi lugha lengwa kwa njia yenye kasoro. Matokeo yake huwa matumizi ya lugha kuwa na kasoro katika kiwango cha fonolojia. Michakato ya kifonolojia ambayo ilidhihirika maneno anuwai yaliyotumiwa na watafitiwa husika katika insha tulizozichunguza ni: udondoshaji na uchopekaji

2.5.1 Udondoshaji

Udondoshaji ni hali ya kuondoa kipashio katika neno kwa njia ambayo inakiuka taratibu za lugha husika. Tofauti katika utaratibu wa mfuatano wa sauti katika uundaji wa maneno kati ya lugha ya kwanza na ile ya pili zilisababisha kudondoshwa kwa sauti au hata silabi nzima kwa njia iliyoleta kasoro katika maneno mbalimbali. Makosa ya udondoshaji yalijitokeza katika mifano ifuatayo:

Insha iliyoandikwa na mwanafunzi mzawa wa Kikamba ilidhihirisha athari ya lugha hiyo katika uendelezaji wa maneno ya Kiswahili kupitia udondoshaji wa sauti pale ilipostahili kutumika. Kutokana na uchanganuzi wa insha za wanafunzi husika, mifano inayodhihirisha kasoro hii ni:

Udondoshaji	Sahihi
[pu^de si pu^de]	punde si punde
[we^zenu]	wenzenu
[kiwa^ja]	kiwanja

Katika mifano hii yote, nazali /n/ ndiyo imedondoshwa; na hivyo, kuleta upungufu katika maneno husika. Kosa hili lilijitokeza katika sauti mwambatano ambazo zilistahili kuwapo ili maneno hayo yakubalike katika Kiswahili Sanifu. Sauti mwambatano ambazo ziliathiriwa na

udondoshaji huo ni: nd, nz, na nj. Wazawa wa Kikamba hutatizwa na nazali zinapotakiwa kuambatanishwa na sauti nyingine ili kuunda sauti mwambatano. Hili ni tatizo ambalo lina chanzo chake katika usahihishaji uliokithiri ambapo mtafitiwa aliposhindwa kung'amua ni wapi pa kutumia nazali husika na kinyume chake, aliamua kuidondosha.

Katika insha za watafitiwa wa jamii-lugha ya Kikisii, udondoshaji uliojitokeza ulihusu /h/. Udondoshaji ulitokea katika mazingira ambamo irabu mbili zimetumika na kuhitaji fonimu hiyo itokee katikati yao. Mifano ya udondoshaji huu inadhihirika katika maneno yafuatayo:

Udondoshaji	Sahihi
[asubu^I]	asubuhi
[wame^aribu]	wameharibu
[wata^iniwa]	watahiniwa

Hali hii imetokana na sauti /h/ kutopatikana katika Kikisii. Ukosefu wa sauti hiyo huwafanya wazawa wa jamii-lugha husika kutoitumia pale inapostahili kutumiwa

2.5.2 Uchopekaji

Uchopekaji ni mchakato wa kifonolojia unaorejelea hali ambapo kipashio huongezwa katika neno. Matokeo ya hali hii ni kuvyazwa kwa neno ambalo linasheheni sauti ya ziada ambayo haikuwapo katika neno la msingi

Katika insha iliyoandikwa na mwanafunzi mzawa wa Kikamba, maneno mbalimbali yaliendelezwa vibaya kutokana na uchopekaji wa sauti zisizohitajika. Maneno yanayodhihirisha uchopekaji huo ni pamoja na:

Uchopekaji	Sahihi
ndukani	dukani
uchanguzi	uchaguzi
sembuleni	sebuleni
hili tupate	ili tupate

sitahisahahu sitaisahau

Katika mifano mitatu ya kwanza, mtafitiwa husika alichopeka sauti nazali mahali isipohitajika. Uchopekaji huo ulivyaza sauti mwambatano /nd/, /ŋ/ na /mb/ ambazo zimetumika katika mazingira yasiyofaa. Hali hii ilitokana na tatizo la sauti mwambatano kwa wanafunzi wazawa wa Kikamba ambao hawajui ni wapi inapaswa kutumiwa na kinyume chake Mifano miwili ya mwisho nayo ilidhihirisha uchopekaji wa /h/ katika maneno mawili husika. Tatizo hili limejitokeza katika mazingira ambamo irabu pekee ingetumiwa. Haya ni mazoea ya wanafunzi wazawa wa Kikamba ambapo mara nyingi irabu ikitokea peke yake huchopekewa /h/ bila kugundua kuwa hali hiyo huleta hitilafu katika matumizi ya lugha. Uchopekaji huo ulijitokeza katika mazingira yoyote ambamo irabu ilitokea kama silabi kamili. Katika neno hili, uchopekaji wa /h/ ulitokea mwanzoni ambapo /i/ ilitahili kuwa silabi iliyojismamia. Neno *sitahisahahu linaonesha namna /h/ imechopekwa mara mbili – katikati na mwishoni mwa neno. Uchopekaji wa kwanza umetokea kabla ya /i/ ilhali wa pili umetokea kabla ya /u/. Tatizo la uchopekaji wa sauti kwa njia pungufu lilidhihirika pia katika insha za watafitiwa wazawa wa Kikisii. Uchopekaji ulitokea zaidi mwanzoni mwa maneno na kwa kiasi katikati mwa maneno. Mifano iliyodhihirisha kasoro hii ni:

Uchopekaji	Sahihi
Inchi ya Kenya	nchi ya Kenya
hule	ule
huamusi	uamuzi
masikini	maskini

Katika mfano wa kwanza, uchopekaji wa irabu /i/ mwanzoni mwa neno husika ulitokana na mazoea ya watumiaji wa Kikisii wa kuanza maneno hususani nomino kwa irabu. Ni nadra kupata maneno ya Kikisii yakianza kwa konsonanti. Kwa mfano nomino nchi kwa Kikisii ni ense. Hali hii ndiyo imehamishiwa katika uendelezaji wa maneno ya Kiswahili. Matumizi ya irabu mwanzoni mwa maneno mbalimbali na wazawa wa Kikisii hunuiwa kurahisisha utamkaji wa maneno husika. Nayo mifano ya pili na tatu, imesheheni uchopekaji wa /h/ mwanzoni mwa maneno husika. Kasoro hii inatokana na matamshi ya wazawa wengi wa jamii-lugha ya Kikisii

hususani katika maneno yanayoanza kwa irabu. Mara nyingi /h/ huongezwa mwanzoni wakati wa kutamka maneno ya aina hiyo. Kasoro hiyo ndiyo huhamishiwa kwenye maandishi kama ilivyotokea katika insha za watafitiwa wa jamii-lugha hiyo. Hatimaye katika mfano wa mwisho, mtafitiwa amechopeka /i/ katikati ya konsonanti mbili kwa sababu mfuatano huo haukubaliki katika lugha yake ya kwanza. Kikisii kama zilivyo lugha nyinginezo za Kibantu, hutumia mfuatano wa KI mara nyingi katika uundaji wa maneno. Hali hii ndiyo imehamishiwa katika Kiswahili kwa njia inayoleta kasoro.

2.6 Msingi Wa Nadharia

Nadharia Ya Uchanganuzi Makosa (UM)

Watafiti walitumia nadharia hii kwa sababu athari za lugha ya kikikuyu (L1) katika kujifunza Kiswahili (L2) ni wazi. Makosa ya kisarufi, matumizi ya msamiati na utamkaji sahihi imeangaziwa vyema sana katika nadharia hii *yathe significance of learner`s errors*

Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UM) ambayo ilizungumziwa kwanza na Stephen Pit Corder (1967). *The significance of learner`s errors*, na kupata mwelekeo mnamo miaka ya 1970. Nadharia hiiinaangazia makosa anayofanya mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili. (Gas na Selinker 2008). Nadhari ya uchanganuzi makosa hutumiwa na watafiti kuonyesha makosa yanayofanywa na wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili. Nadharia ya uchanganuzi makosa huchunguza aina ya makosa na vitu vinavyosababisha makosa hayo. Corder (1967) anabainisha misinga ya nadharia yake kama ifuatavyo.

Wakati wanafunzi wanapojifunza L2, lazima wanafunzi wafanye makosa

Mwanafunzi anapofanya makosa asiathibiwe kwani ni kawaida katika ujifunzaji wa lugha ya pili na anapendekeza hatua zifuatazo; kutambua makosa, kuyaainisha kisha kutafta mbinu mwafaka za kurekebisha makosa hayo.

Corder (1967) anaainisha hatua zifuatazo ambazo mtafiti anafaa kufuata katika uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi,

1. Kukusanya sampuli ya kazi ya wanaojifunza lugha ya pili. Kama vile insha

2. Kutambua makosa kama vile ya matamshi au matumizi yasiyofaa ya msamiati au kupanga viambishi kusiofaa katika sentensi.

Kueleza jinsi wanafunzi wamesababisha makosa hayo katika matumizi ya lugha.

Kuhesabu makosa ya kila mwanafunzi na kuyaweka makosa hayo katika vikundi.

3. Kutambua vipengele vyenye matatizo. Vipengele vya lugha vinavyowatatiza wanafunzi na kusababisha makosa hutambuliwa. Kwa mfano, fonimu fulani, virejeshi, vitenzi, nyakati, miundo ya silabi na kadhalika.
4. Kufafanua chanzo cha makosa anayofanya mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili.
5. Kuyasahihisha makosa anayofanya mwanafunzi ili kujua jinsi ya kukabiliana na makosa hayo.
6. Kuonyesha athari inayosababishwa na makosa hayo.

2.7 Mapengo Ya Utafiti

Watafiti mbalimbali wamechunguza juu ya athari za L1(lugha ya kwanza)katika kujifunza L2 (Kiswahili). Watafiti wengi wamekuwa wakieleza mapungufu kuhusu athari ambazo zimejitokeza katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Kufikia sasa, hakuna thibitisho ya kuonyesha kwamba kumefanywa utafiti kuhusu athari za lugha ya kikikuyu katika kujifunza lugha ya Kiswahili katika kaunti ndogo ya Othaya, kaunti ya nyeri, Kenya.

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI

Utangulizi

Katika sura hii watafiti wameangazia: mbinu za utafiti, eneo la utafiti, idadi ya walengwa, mbinu ya kuteua sampuli na vifaa vya utafiti. Watafiti pia wanaangazia uhalali wa utafiti, mbinu za ukusanyaji data na maadili ya kuzingatiwa katika utafiti.

3.1 Mbinu Za Utafiti

Watafiti walizikusanya data kwa kutumia njia shirikishi. Watafiti walitumia mbinu ya mazungumzo ya moja kwa moja na walengwa ili kubaini iwapo lugha ya kwanza huathiri matamshi yao. Watafiti pia walitumia uandishiwa insha ili wabaini iwapo wanafunzi wa shule hizi teule wana uwezo wa; kuwa na upatanisho sahihi wa kisarufi, matumizi yafaayo ya msamiti na utamkaji ufaao wa sauti za lugha ya Kiswahili.

3.2 Eneo La Utafiti

Utafiti huu utafanywa kaunti ndogo ya Othaya, Kaunti ya Nyeri, Nchini Kenya. Hili ni eneo ambalo wakaazi wake wengi ni wazungumzaji asilia wa lugha ya Kikikuyu.

3.3 Idadi Ya Walengwa

Kulingana na takwimu za baraza la mitihani nchini Kenya (KNEC), Kaunti ndogo ya Othaya ina shule 34. Watafiti walilenga wanafunzi 3,715 ambao ni wanafunzi wa wa kidato cha nne.

3.4 Uteuzi Wa Sampuli

Walilengwa na utafiti huu ni wanafunzi na walimu wa Kiswahili katika shule zilizoteuliwa kwa kutumia mbinu za uteuzi wa sampuli mpangilio na uteuzi wa maksudi. Watafiti waliteuwa shule tano za kutwa na shule tano za bweni katika kaunti ndogo ya Othaya.

Katika kuteua sampuli ya wanafunzi, pendekezo la Glen (2013) *10% condition in statistics* linalosema kuwa ifadi ya sampuli isizidi asilimia 10, wakati wowote tunapotumia sampuli katika utafiti, sampuli hiyo isizidi asilimia 10, hivyo watafiti walitumia asilimia 3.0 ya walengwa

Kitengo	Shule za Kutwa	Shule za Bweni	Jumla	Sampuli iliyoteuliwa
Wanafunzi	1024	2641	3715	60

Vifaa Vya Utafiti

Utafiti huu utatumia vifaa vifuatavyo:

3.5.1 Insha

Watafiti walitumia uandishi wa insha kama kifaa cha kwanza cha kukusanya data. Watafiti waliwateua wanafunzi walioshirikishwa katika uandishi wa insha na kisha kuwapa mada katika uandishi walioindikia bila kupimiwa muda.

Baada ya hapo watafiti waliwapa wanafunzi hao insha hizi wazisome kwa sauti huku watafiti wakinakili makosa ambayo yalijitokeza katika uandishi huo.

3.5.2 Ushiriki

Katika kitengo hiki watafiti waliwagawa wanafunzi katika makundi mawili kisha kuwapa mada ya kujadili ili watathmini uwezo wa wanafunzi hao katika utunzi wa sentensi sahihi na matumizi yafaayo ya msamiati. Watafiti walishiriki katika mada ibuka ambazo wanafunzi hawa walikuwa na ufahamu nazo

3.6 Mbinu Za Ukusanyaji Wa Data

Watafiti walitumia mbinu ya ushiriki na uandishi wa insha.

3.7 Mbinu Ya Uchanganuzi Wa Data

Watafiti walitumia mbinu ya maelezo katika uchanganuzi wa data baada ya kutoka nyanjani. Athari ya kikikuyu katika kujifunza Kiswahili sanifu kisha athari zingine zifuate mmoja baada ya ingine. Watafiti walitumia nadharia ya uchanganuzi makossa (UM).

3.8 Maadili Ya Kuzingatiwa Katika Utafiti

Watafiti walilenga kufanikisha utafiti wao watazingatia maadili ya watafitiwa ili kutoa taarifa za kweli bila ya woga. Kwa mujibu wa Sture (2010) mkabala wa uhalali ni mojawapo ya maswala muhimu ambayo watatafiti wanapaswa kuyazingatia kwa uzito wakati wakifikiria, wakipanga, kutekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wao. Anazidi kufafanua kuwa haki ya mtafitiwa ni kuhakikisha usalama wake, haki ya kujua madhumuni, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swali atakavyopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti.

3.9 Uhalali Wa Utafiti

Watafiti walitumia kibali walichopewa na chuo na kuomba vibali kutoka kwa serikali ya kaunti ndogo ya othaya ili kujitambulisha na kuwahakikishia usalama wa taarifa zao. Watafiti wataomba ruhusa ya kutoka kwa vitengo vyote vinavyoshughulika na maswala ya elimu katika kaunti ndogo ya Othaya ili kufanya utafiti wao. Watafiti kisha wataomba ruhusa kutoka kwa walimu wakuu na walimu ili kuwatumia wanafunzi hawa katika utafiti wao kwani ndiyo wazazi wao shuleni.

SURA YA NNE: MATOKEO NA MAJADILIANO

4.1 UTANGULIZI

Katika sura hii, watafiti walingazia matokeo ya utafiti wao. Matokeo ya utafiti wenyewe yaliwasilishwa kwa kutegemea malengo yafuatayo:

- i) Kubaini namna Kikikuyu kinavyoathiri uwezo wa wanafunzi wa kutumia upatanisho sahihi wa kisarufi katika sentensi katika shule za upili, Kaunti Ndogo ya Othaya, Nyeri, nchini Kenya.
- ii) Kuweka wazi athari za Kikikuyu kwa uwezo wa wanafunzi wa matumizi yafaayo ya msamiati katika shule za upili, Kaunti Ndogo ya Othaya, kaunti ya Nyeri, nchini Kenya.
- iii) Kutambua namna Kikikuyu kinavyoathiri uwezo wa wanafunzi wa utamkaji ufaao wa sauti za Kiswahili sanifu katika shule za upili, Kaunti Ndogo ya Othaya, Kaunti ya Nyeri, nchini Kenya.

4.2 Kiwango Cha Upokezi Wa Majibu Ya Wahojiwa

Wanafunzi kutoka shule mbalimbali zilizoteuliwa waliandika insha (licha hawakuandika kwa umakinifu kwa sababu haukuwa mtihani) na kuzirejesha zote ambayo ilikuwa ni asilimia 100. Kulingana na Berge (2016), asilimia 70 ya majibu yaloyopokelewa kutoka kwa watafitiwa ni bora kuchanganuliwa kufanikisha utafiti.

Kitengo	Zilizopeanwa	Zilizorejeshwa	Asilimia
Wanafunzi	66	58	89

4.3 Uchanganuzi Wa Data

Katika utafiti huu, watafiti walizipa shule majina ya msimbo A, B, C, D, E, F, G, H na kisha kutotumia majina halisi ya wanafunzi ya na hivyo kuzipa insha zilizoandikwa msimbo 1, 2, 3, 4, 5,6 ili kuziweka insha hizo kwenye mizani sawa wakati wa kuzichanganua data.

4.4 Upatanisho Sahihi Wa Kisarufi.

Upatanisho sahihi wa kisarufi ni utaratibu wa kimuundo ambao nomino za Kiswahili sanifu huwakilishwa na mofu teule katika vipashio vinavyohusiana nayo katika tungo za kiswahili (BAKITA) 2016. Upatanisho huu wa kisarufi hupania kuleta uwiano au ukubalifu katika tungo kati ya nomino, kiima na vipashio vingine vinavyoambatana kwenye utungo huo, Ili kuleta mantiki na maana inayoeleweka vyema na msomaji.

Katika utafiti huu ambapo watafiti wamechunguza athari zalugha ya kikikuyu katika kujifunza Kiswahili sanifu, wamezisoma insha na kufuatilia majadiliano walikuwa nayo na wanafunzi wa kidato cha nnewalioteuliwa kushiriki katika utafiti huu na kubaini makosa yafuatayo ya upatanisho ambao si sahihi wa kisarufi za Kiswahili sanifu.

Kosa la upatanisho	Kipashio kisicho sahihi	Usahihi
Mtoto hu <u>o</u>	{o}	Mtoto huyo
Sitaenda shu <u>r</u> eni	{r}	Sitaenda shuleni
Nilifuh <u>l</u> ahia sana	{l}	Nilifurahia sana
Na hi <u>y</u> o uvumi	{iy}	Na huo uvumi
Ndugu <u>y</u> a familia ya mwangi wa Moruu	{ya}	Ndugu wa familia ya mwangi wa Moruu
Wake* <u>z</u> ao waliwasili kwa fujo	{z}	Wanawake wao waliwasili kwa fujo
Kuishi kwingi ndiko kuona <u>k</u> wingi	{kwi}	Kuishi kwingi ndiko kuona mengi

Kutokana na jedwali hili, neno lenye alama ya kinyota (*) si neno la Kiswahili sanifu na limetumika visivyo katika sentensi. Wanafuzi ambao lugha yao ya kwanza ni kikikuyu walifanya waliyafanya haya makosa, si kimaksudu tu bali ni ule uhamishaji wa umilisi wa lugha yao yakwanza moja kwa moja katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

Data iliyowasilishwa katika jedwali hilo (hapo juu) linadhihirisha kuwa watafitiwa wameyafanya haya upatanisho wa kisarufi mara kwa mara katika maandishi na kuzungumza kwao, yaani mofu zilizoekwa katika mizizi ya maneno haziafiki nomino zinazorejelewa hivyo basi kukosa upatanisho wa kisarufi ufaao. Makosa haya ya yamefanywa na wanaafunzi wenye asili ya kikikuyu ambao waliandika insha na kushirikia katika utafiti.

Matatizo haya ya upatanisho usiyo sahihi unaweza kuwa umesababishwa nahali ya ugeni wa dhana, hali ya kuiga kutoka kwa walimu wao au watu katika jamii wanamotoka wanafunzi hawa. Pia hali ya kiakili wanapoandika au kuzungumza inaweza changia katika kutokea kwa matatizo haya ya usahihi wa vipatanishi vya kisasarufi vinavyofaa.

4.5 Matumizi Yafaayo Ya Msamiati

Msamiati ni orodha ya maneno ambayo binadamu huyajua na kuyatumia katika shughuli zake za kila siku. Watafiti walichunguza chinzi wanafunzi wenye asili ya kikikuyu wanatumia maneno katika uandishi wa insha na katika mitakusano yetu nao. Watafiti wamezisoma na kuyaangazia makosa ambayo wanafunzi hao wameyafanya. Watafiti waliyaweka makosa hayo katika makundi yafuatayo.

4.5.1 Ubadilishaji Fonimu

Wanafunzi wa asili ya kikikuyu wametumia fonimu fulani mahali ambapo fonimu nyingine sahihi inastahili kutumiwa. Kosa hili la ubadilishaji wa fonimu bila shaka ni tofauti na lile la uchopekaji kwa maana kwamba kipashio kilichojumuishwa katika nafasi hiyo hakifai kuwapo, kipashio kinastihili kuambikwa mahali hapo.

Ubadilishaji	Sahihi
Nilifulahi	Nilifurahi
Lile lol <i>ī</i>	Ile lori

Ka <u>l</u> o	Karo
<u>R</u> isaa rimoja	Lisaa limoja
A <u>r</u> inegua kiuno	Alinengua kiuno
Mche <u>r</u> e	Mchele
Jitaya <u>l</u> ishe	Jitayarishe
Shini	Chini
Shai	Chai
Chati	Shati
Washa	Wacha

Katika jedwali hili, wanafunzi wa asili ya kikikuyu walitumia /r/ ambayo kimadende cha ufizi na badala yake kutumia /l/ ambayo ni kitambaza cha ufizi. Makosa haya yametokana na ukweli kwamba wakikuyu hawana /l/ (otiende 2013). Lakini ukweli huu unabadilishwa pale ambapo wanatumia /l/ mahali wametakiwa kutumia /r/.

Wanafunzi hawa pia wametumia /sh/ ambacho ni kikwamizo cha kaaka gumumahali ambapo wametakiwa kutumia /ch/ kipasuo kwamizo cha kaa kaa gumu. Lakini tena wanafunzi hawa wametumia /ch/ mahali ambapo wanatakiwa kutumia /sh/.

4.6 Utamkaji Ufaao Wa Sauti Za Kiswahili

Katika sehemu hii ya utamkaji ufaao wa sauti za Kiswahili, watafiti wametumia insha zilizoandikwa kwani katika insha hizo wanafunzi wenye asili ya kikikuyu waliandika maneno mbalimbali jinsi ambavyo wao huyatamka. Katika utafiti huu pia, watafiti walishiriki katika majadiliano na wanafunzi wa shule zilizoteuliwa kwa umakini huku wakiandika makosa ya utamkaji ambayo yalitokea na kuendelezwa na wanafunzi hawa.

Katika kuchanganua data hizo, watafiti walichunguza makosa hayo ya utamkaji na kuyaweka katika makundi yafuatayo.

4.6.1 Udondoshaji

Udondoshaji ni ile hali ya kutoa au kuondoa kipashio fulani katika neon kwa njia ambayo kwa namna fulani uathiri neon hilo. Watafiti katika uchunguzi wao wamebaini kwamba wanafunzi wenye asili ya kikikuyu hukumbwa na tatizo hili katika mawasiliano nahata pia katika uandishi wao. Makosa yafuatayo ya udondoshaji yamejitokeza katika utafiti.

Udondoshaji	Sahihi
M [^] gulumo	Mngurumo
Tuli [^] goja	Tulingoja
Aline [^] gua	Alinengua
Aliyeniku [^] buka	Aliyenikumbuka
Wamea [^] biwa	Wameambiwa
[^] bali	Mbali
A [^] bacho	Ambacho
Nyu [^] ba	Nyumba
G [^] afla	Ghafla
Kunis [^] taki	Kunishtaki
Pu [^] de si pu [^] de	Punde si punde
Kuvu [^] ja	Kuvunja
Majo [^] zi	Majonzi

Katika jedwali hili, makosa ya udondoshaji yamefuata ruwaza fulani kwani ni nazali pekee zimedondoshwa katika sauti mwambatano. Kutokana na mifano hii sauti mwambatano zenye nazali zilizoathiriwa ni: /mb/, /nʃ/, /nz/, /nd/ na /ns/. Tatizo la utamkaji wenye kasoro limehamishiwa katika maandishi ya maneno husika. Nalo neno ***kustakiwa**, linadhihirisha kudondoshwa kwa sauti /h/ ambayo inatakiwa kutokea baada ya /s/ ili kuunda sauti /ʃ/. Vivyo hivyo sauti /ʒ/ inayotakiwa kutumiwa katika neno **gamu**, ni tatizi kwa wanafunzi wazawa wa Kikikuyu kutokana na hali kwamba ni nadra sauti hiyo kutokea katika Kikikuyu.

4.6.2 Uchopekaji

Uchopekaji ni mchakato wa kuongeza kipashio katika neno. Katika insha zilizoandikwa na wanafunzi wenye asili ya kikikuyu waliunda maneno ambayo yalisheheni sauti zaidi ambazo hazikuwepo kwenye maneno ya msingi. Wanafunzi hawa katika mazungumzo yao na watafiti, waliendeleza uchopekaji mwingi ambao watafiti wameutumia katika kuandaa jedwali lifuatalo.

Uchopekaji	Sahihi
Umew <u>and</u> ia	Umewadia
Ma <u>nd</u> awa	Madawa
<u>N</u> janga	Janga
A <u>m</u> kuwa	Amkuwa
Ku <u>m</u> ula	Kumla
Ku <u>m</u> wacha	Kumwacha
Shule <u>e</u>	Shule
<u>I</u> nchi	Nchi
<u>M</u> basi	Basi

Katika mifano ya kwanza miwili, watafitiwa walichopeza /nd/ hivi kwamba wameunda sauti mwambatano ambazo hazikustahili kuchopezwa katika maneno hayo. Wanafunzi wametumia sauti mwambatano /nd/ badala ya /d/.

Vilevile wanafunzi walichopeza /u/ kwenye maneno; ***amuka**, ***kumula** na ***kumuwacha** katika mazungumzo yao. Pia neno ***shulee** lilirefushwa kwa kuongezewa /e/ ambayo haipo katika matamshi ya Kiswahili sanifu. Pia /i/ imechopezwa kwenye neno ***inchi** na vilevile /m/ kuongezwa kwenye neno ***mbasi**.

SURA YA TANO: MHUTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Katika sura hii, watafiti waliangazia mhutasari wa matokeo walihitimisha na kutoa mapendekezo yao. Kisha walitoa mapendekezo ya tafiti zaidi kuhusiana na mada hii.

5.1 Mhutasari wa utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza athari za kikikuyu katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu kaunti ndogo ya Othaya kaunti ya Nyeri Kenya. Jumla ya wanafunzi 66 waliandika insha na kushirikiswa na watafiti bila kuwaambia wanafunzi hawa moja kwa moja kwamba makosa yao ua utamkaji ufaao wa sauti za Kiswahili sanifu, matumizi yafaayo ya msamiati na upatanisho sahihi wa kisarufi yanachunguzwa. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UM). Utafiti huu ulingozwa na maswali matatu. Katika harakati za kushughulikia utafiti huu, watafiti waliuweka utafiti wenyewe katika sura tano.

5.1.1 Upatanisho sahihi wa kisarufi

Kutokana na data zilizokusanywa na kuchanganuliwa kutoka shule zilizoteuliwa, inadhihirika wazi kuwa asilimia themanini na sita nukta tatu (86.3) walikumbwa na tatizo hili la utaratibu wa kimuuundo ambao nomino za Kiswahili huwakilishwa na mofu fulani katika kujifunza Kiswahili sanifu. Makosa haya yalionekana katika insha za wanafunzi na pia katika majadiliano baina yao na watafiti.

5.1.2 Matumizi Yafaayo Ya Msamiati

Katika matumizi yafaayo ya msamiati, wanafunzi wengi ambao walishiriki katiak majadiliano na uandishi wa insha wamekubwa na matatizo katika kuutumia msamiati wa Kiswahili. Asilimia kubwa ya watafitiwa wamekumbwa na matuzimi yasiyofaa ya msamiati wa Kiswahili. Pia ilidhihirika kwamba wengi wa wnanafunzi hawa walibalisha fonimu fulani na hivyo kuyaendeleza maneno mengi visivyofaa.

5.1.3 Utamkaji Ufaao Wa Sauti Za Kiswahili Sanifu

Hapa wanafunzi walifanya makosa ya kudondosha na kuchepeza fonimu, mofu silabi au hata neno katika maneno ambayo yalifaa kutamka vinginevyo. Aidha ulinganifu wa lugha ya kikikuyu na Kiswahili ambazo ni lugha za kibantu ulichangia sana katika utamkaji usiofaa. Hili ndilo lilichangia katika asilimia kubwa ya wanafunzi kukabiliwa la utamkaji ufaao kuliko tatizo

lingine, kwa sababu hii takriban asilimia tisini na nane (98%) yya wanafunzi walioshiriki katika utafiti huu wlikumbwa na makosa ya utamkaji ufaao wa sauti zakiswahili sanifu.

5.2 Hitimisho Ya Utafiti

Kwanza kabisa ni vye ma kutaja kwamba utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Hii ni nadharia ambayo husaidia kutambua makosa na kuyarekebisha. Katika utafiti huu, watafiti wametambua makosa ya Kiswahili yaliyosababishwa na athari ya lugha ya kikikuyu wakati wa wasemaji wa lugha ya kikikuyu wanapojifunza lugha ya Kiswahili sanifu kama lugha ya pili.

Kutokana na matokeo ya utafiti, nadharia tete zote zilikubaliwa. Matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba; kikikuyu kinaathiri uwezo wa wanafunzi wa kutumia upatanisho sahihi wa kisarufi katika sentensi za Kiswahili sanifu katika shule husika kaunti ndogo ya Othaya. Matokeo yanaonyesha kwamba kikikuyu kinaathiri uwezo wa wanafunzi kutumia msamiati ufaao mazungumzo na uandishi katikiakaunti ndogo ya Othaya. Kikikuyu kinaathiri uwezo wa wanafunzi wa utamkaji ufaao wa sauti za kiswahili sanifu kaunti ndogo ya Othaya.

5.3 Mapendekezo Ya Utafiti

Kupitia kwa mihimili mwafaka ya nadharia ya uchanganuzi (UM) ambayo iliongoza watafiti katika utafiti huu, wamebaini kuwa lugha ya kwanza ina nafasi kubwa sana katika kujifunza lugha ya pili, kutokana na ukweli huu, kuna haja ya ya walimu kuelewa jinsi L1 inavyoathiri uwezo wa wanafunzi kujifunza L2. Pia watafiti wanapendekeza kwamba tafiti zifanywe kuhusu hatua ambazo walimu wa kiswahili wanaweza kuchukuwa katika kupunguza athari za kikikuyu katika utaufaao wa Kiswahili sanifu

Wahandisi wa lugha ya Kiswahili ambao wamefanya tafiti za kiisimu katika jamii ya kikikuyu na ambao wana stadi za umilisi wa Kiswahili waandae makala ambayo yalitumiwa wa waandishi ambao waliainisha makosa yanayofanywa na wanafunzi wa kikikuyu na kisha kuyachapisha makala hayo. Makala hayo yaandamane na picha zinazoeleza dhana hizo na kisha zitumiwa katika kufunzia wanafunzi kuanzia chekecheche hadi gredi ya sita katika mtaala mpya wa elimu nchhini.

Utafiti huu ulijikita katika kuonyesha athari za lugha ya lugha ya kikikuyu katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu lakini haukungazia kiini cha makosa haya katika lugha, kwa hivyo watafiti

wanapenekeza utafiti kufanywa kuchunguza kiini cha makosa haya ambayo yanafanywa na wanafunzi katika eneo hili la utafiti.

Ni muhimu kutambua kuwa katiba ya Kenya ina zaidi ya jamii lugha 42. Utafiti huu uliegemea zaidi kwenye nadharia ya Uchunganuzi Makosa (UM) na wanafunzi wakikuyu. Kutokana na ukweli kuwa wanafunzi kutoka jamii lugha mbalimbali hufanya makosa tofauti, kuna hitaji la tafiti zingine kufanywa kwenye wanafunzi wenye L1 nyingine kwa kutumia nadharia zingine ili kutambua makosa hayo. Baada ya kutambua makosa hayo pendekezo la watafiti katika aya ya pili chini ya mada hii (mapendekezo ya utafiti) yafuatwe ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wanakua na kuwa na umilisi halisi wa picha.

Vitabu vya fasihi andishi viongezwe katika shule za upili ili kuwasaidia wanafunzi kusoma na kukuza msamiati wao wenyewe. Katikashule hizi walimu wajitolee mhanga wa kuhakikisha kwamba wanafunzi hawa wanasoma bila kuweka makosa ya utakmaji na hivyo watasaidika kwani kosa la utakmaji ndilo lililokumba wengi wa wanafunzi wengi ambao walikinajisi Kiswahili katika kutamka kwao

5.4 Mapendekezo Zaidi

Utafiti huu hauwezi kudai kwamba ulishughulikia athari za kikikuyu katika kujifunza Kiswahili sanifu ila tuna matumaini kwamba tafiti zingine zitaweza kutalii maswala haya na mengine kama vile kila swali la utafiti huu lichukuliwe na kuwa mada ya utafiti ili kuafiki mawanda mapana ya athari hizi na kiini chake.

Tafiti zingine zifanywe kuanzi kwa fenitiki, fonolojia, mofolojia, sintaksia semantiki na pragmantiki kwa ukamilifu juu ya jamii lugha hii na jamii lugha zote nchini ili kuondoa matatizo yote yanayokumba Kiswahili sani

MAREJELEO

- Athanasopoulos, P.(2011) *Language and bilingual cognition*. In Cook, V. & Bassetti, B. (eds.). *Language and Bilingual cognition*Hove: Psychology Press
- Athanasopoulos, P. & Bylund, M. (2013). The 'thinking' in thinking for speaking. *Language*,
- Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam University Press.
- Corder, S. P. (1967). *Error Analysis and Interlanguage*. Oxford University Press.
- Gass, S. & Selinker, L. (1994). *Second Language Acquisition: An Introductory Course*. In N. AbiSamra (2003) *An Analysis of Errors in Arabic Speakers' English Writings*.
- Kisakwah M.A. (2014). Uchanganuzi makosa na muundo wa sentensi za Kiswahili.Tasnifu M.A. Chuo kikuu cha Nairobi (UON).
- Lakkis, K. naMalak, M. A. (2000). Understanding the Transfer of Prepositions. *Forum, Vol 38, No 3*. Retrieved in May 22nd, 2007 from <http://exchanges.state.gov/forum/vols/vol38/no3/p26.htm>.
- Mangwa, D. O. (2005).*Athariza Kikisii katika Kiswahili na Zinavyochangia MatokeoMabayaya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili kwa Wanafunzi Wakisii Wilayani Kisii Kusini*. Tasnifuya M.A (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya
- . Massamba, D. P. B. (1986). On the Influence of Local Languages on Kiswahili: The Case of Mara Region in Tanzania. *Kiswahili*, 53/1 na 53/2, 67-83.
- Masasa, M.A. (2017) Athari ya matamshi ya lugha ya Kijita katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mochiwa, Z. M. (1979). *The Impact of Kiswahili Language on Ethnic Languages: A Case Study from Handeni District*. Tasnifuya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.
- Mudhune, E. S. (1994). A Contrastive Analysis Approach to the Learning of Swahili Morphosyntax by Luo Speakers.
- Ndungu ,I. (1999) *Kikuyu Learners of English as Second Language*: Tasnifu ya Uzamifu: Nairobi: UON.

- Ngugi, J. (2007) Uchunguzi wa Taathari za Kifonolojia miongoni mwa Wanafunzi Wagikuyu : Mfano kutoka Tarafa ya Bahati, Nakuru. Tasnifu ya Uzamili (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya
- Nunan, D. (1992)*Research Methodology in Language Learning*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Obara. J. M. (2014). Uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na Wanafunzi wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii. Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).
- Otiende, M. A. (2013) Athari za mofolojia ya Kibasuba katika matumizi ya Kiswahili Kama Lugha ya pili. Tasnifu ya M.A. (UON).
- Olive, M. na Abel, G. (2011) *Research Methods: Quantitative and Qualitative approaches*. Nairobi: Acts Press
- Onyango, J. (1997) Uziada wa Kisarufi katika Kiswahili cha Wanafunzi wa Kinyala: Mtazamo wa uchanganuzi Linganuzi. Tasnifu ya Uzamili (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.
- Pia, J. (1965) Somali Sound and Inflections. (Unpublished PhD), Indiana University, Bloomington, United States of America. 86
- Prasad, T. (2012) *Acouse in Linguistics*. New Delhi: PHI Learning Private Limited.
- Rapondo, M. (2005) Makosa ya Kimofosintaksia yanayojitokeza katika kazi za Kiswahili zilizoandikwa
- Saeed, J. (1999) *The Focus Structure of Somali*. Philadelphia :John Benjamins Publishing.
- Schane, S. (1973) *language Change and Generative Phonology*. Oxford: Oxford University Press.
- Selinker, L. (1972) *Inter Language*. New York: Rawlence erlibaum associates, INC (RAL).
- Sture, J. (2010) *Ethics in Research Project*. Some Guidance on Recognising and Addressing Ethical Issues. Bradford: University of Brandford Press.

- Taylor, B. (1975) The Use of Overgeneralization and Transfer Learning Strategies by Elementary and Intermediate Students of ESL. *Language Learning*, 25:73- 107 .Retrieved in June 7th,2008 from abisamra03. tripod. com/nada/languagea cq-erroranalysis.html.
- Van Els, T. et al (1984) *Applied Linguistics and the Learning and Teaching of Foreign Languages*. . London: Edward Arnold.
- Willis Y. na David O. (2011). *A General Guide to Writing Research Proposal and Report*. Jomo Kenyatta Foundation.
- Yule, G. (1985) *The Study of Language*. London: Cambridge University Press

VIAMBATISHO

Kiambatisho I: Barua ya Ombi la Kukusanya Data



Kwa Bw./Bi.,

KUH: MAOMBI YA KUKUSANYA DATA

Watafiti, Vincent wanjala, Evans Oginga na Frevian Mwaura ni wanafunzi wa kozi ya ualimu Chuo Kikuu cha Greta. Watafiti wanatafitia athari za Kikikuyu katika kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu katika shule za upili kaunti ndogo ya Othaya na watafiti wanaomba kutumia wanafunzi wa kidato cha nne katika shule ya

Hojaji hii itawasaidia watafiti kuboresha na kupata mwelekeo wa utafiti wao. Majibu utakayotoa yatakuwa ni siri na yatatumika tu katika utafiti huu na si kwa njia nyingine ile. Hili ni mojawapo ya mahitaji ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya kwanza. Watafiti wanaomba ruhusa ya kufanya

Majibu yako yatatufaa sana na yatatumika kwa ajili ya masuala ya kiakademia pekee.

Wako waaminifu

.....

Evans Oginga

.....

Wanjala Vincent

.....

Frevian Wanjiku

Uandishi wa insha kwa wanafunzi



Insha kwa wanafunzi

MADA YA UANDISHI: siku ambayo sitawahi sahai

Jina	
Shule	

INSHA 1

SIKU AMBAYO SITAWAISAHAU

Ilikua ni asubuhi na mapema.mama yangu malikuwa mameenda safali ya bali.hivyo hiyo siku nikajiabia sitaenda shureni. Siku hio baba yangu alikua ameniabia kuwa lazima ningejuwakilisha shureni kwa kuwa ilikua siku ya mtihani wa kufunga .

Nililala kabisa kwa kuwa nilifulahia sana kutoenda chuleni. Mchana ikafika na nikacheza na mabeste wangu wasichana na maboys mchezo ambao ulikua ni mtamu sana. Tukacheza tukacheza hadi wakati wa kukula ranch. Nikakula chakula kile abacho nilikua nimepack ya kuenda chulee.

Arafu nikalundi kucheza na marafiki zangu.tukacheza tukacheza hadi masaa ya jioni ambapo mam na dad walikuja. Waliponiuliza kama nilienda shulee nikawaambia yes . Wakaniuliza na kwani leo umetoka mapema aje leo na nimeona pupils wengine classmates shulee nikawaambia hao walikuwa na homework ya teacher ndio maana wakachelewa .

Mama yangu akamligia class teacher kwa kuwa yeye ndiyo ananifundisha subject zote na akasema kwaba Losalita hajakua shulee leo. Mama yangu alikasirika sana. Aliabia baba yangu kuwa sikuenda shule ili nicheze na watoto wale wengine. baba alitoa mshipi Ile yake mrefu na kunipika kama nyoka. Nilikua sana kwa Saba u ya uchungu ule nilikua nasikia .

Mama yangu pia alinichukua na kunipiga na mwiko kile Cha jikoni nililia sana kwa uchungu mwingi . Nikaabia sitakula usiku hio na niede nilale mala moja. Hio ni siku ambayo siwezi kusahau maishani mwangu hata na mandawa.

INSHA 2

SIKU AMBAYO SITAWAHI SAHAU

Niliamka asubuhi na mapema kuelekea shuleni kwani mwarimu wa zamu alikuwa mkali sana. Kabya ya kuamka nilipinduka sana. Mama alikuja na kuniita nitayarishe, niende shuleni. Nilisondeka kitanda taratibu na kisha kuelekea shureni baada ya kunywa chai. Haikuwa rahisi kwangu kukimbia shuleni kwani magoti yangu yalikuwa yameumia siku iliyopita kwenye uwaja Nilipofika kwenye geti, sikumwona mwalimu hapo. Ni kama hakuwa amefika shuleni. Nilipoingia, nilisikia, wewe kijana simama hapo. Sauti ya mngulumo ilisema. Nilishangaa sana kwani sikuwa naSmuwona mtu huyo. Nikasimama tisti.

Nilisikia nyayo zikipanduka kuja upande wangu. Wakati huo nilikuwa nmeshikilia roho mkononi. Pengine alikuwa ni jini. Tatizo ni kwamba hata nilishindwa kugeuka upande mwingine.

Nilisikia kofi zito limenigoga mgogoni likiwa limefuatwa na goto moja. Sikujua nifanye nini. Wanafunzi wenzagu walianza kusheka huku wakishuguria dilishani. Mwarimu aliniaibisha mbele ya malafiki zagu. Mbona hivi? Tokea siku hiyo walinipa jina ya kupaga ati "kishtuki".

Sikulipeda jina hiro. Niliabiwa niende nikafyeka nyasi kwa sababu nilikuwa nimeshelewa. Wakati wa shamcha, sikuletewa chakula uko shabani na mutu yeyote. Hakuna aliyenikubuka. Maisha kwani hayana bahati.

Unalauka mapema na bado unaathibiwa kama mbwa! Nilikosea wapi? Haina neon. Mwenyezi mungu atanitetea siku moja. Tangu siku hiyo nilimchukia sana mwalimu huyo wa zamu ya wiki hiyo.

INSHA 3

SIKU AMBAYO SITAWAHI KUISAHAU

Ilikua siku ya jumamosi , pale niliamka asumbuhi na mapema. Iyo siku ilikuwa siku ya arusi ya ndanda yangu. Alikuwa amepata bean na walikuwa wafunge pingu za maisha.

Nilieda halaka bafuni na kukoga na maji yaliyokuwa baridi shadidi . Kisha nikafaa nguo nguo zangu ambazo zilikuwa laini kama paba

Baada ya hapo nilieda sebuleni kufugua kinywa na nikakunywa Shai ya mkadaa iliyokolezwa sukari.

Wazazi wangu walikuwa wameshajitayalisha na ulikua wakati wa kungoa nanga kuenda kanisani . Gari liliegeshwa haraka na tukafika.

Kasisi aliwaunganisa mahalusi na sherehe zikaanza .waliadihiana kutowahi kuachana . Tulienda hadi pale Sherehe zilikuwa tulikula vyakula vya kila aina si mchere, si viazi, si chapati na vinginevyo . Tulikula hadi tukakinai.

Ama kweli hio siku ilikuwa ya kukata na shoka. Sidhani nitawai isahau maisani mwangu. Tulirudi nyubani tukiwa na furaha sana kama tasa aliyejifungua . Ama kwa kweli sitawahi kuisahau siku hiyo

INSHA 4

Siku Ambayo Sitawahi Sahau

Usiku huo nilikuwa nmelala fofofo baada ya kuwa na shughuli mingi kutokana na usafishaji na upandaji maua kwenye bustani letu. Ghafla bin vu nilishutushwa na mayowe yaliyosikika kwa sauti ya juu kulekea nyumbani kwetu. Nilisimama gaflakitandani mwangu ili kuchunguza mayowe hayo yalitoka wapi.

Nilifungua dirisha ya nyumba yangu ili kuchunguza mayowe hayo yalitokea wazi. Lo! Nilipigwa na butwaa nilipouona umati wa watu umekaribia kwenye nyumba ya mnuna wangu . bila

kupoteza wakati nilifungua mulango wangu huku mtima wangu ukinidunda kwa kasi. Nilijitahidi kusongea kwenye umati umati huo ili kuona ni kitu gani kilichokuwa kikikendelea.

Maswali mengi yalinijaa akilini mwangu kwani nilishangaa nini kilikuwa kimempata mnuna wangu. Nilijaribu niwezavyo kupita katikati ya umati ili kujionea mambo yaliyokuwa yanaendea. Gafla niliona mnuna wangu akiwa amelazwa akiwa amelazwa katikati ya umati akiwa na majeraha mwili mzima na akiwa katika hali mahututi. Nilijiuliza ni nini kile ndugu wangu alikuwa amefanya.

Machozi yalinimiminika nilipomwona mnuna wangu amejeruhiwa. Nilijaribu kuuliwa umati nini kilikuwa kimemfanyikia ndugu yangu. Mama mama alinigombeza kwa sauti ya juu na kunambia familia yetu ilikuwa ni ya watu wezi. Ndugu yangu alikuwa ameptikana akiiba mahindi ya jirani. Nilimwonea imani ndugu yangu kwa uchungu aliokuwa anapitia lakini singeweza kumsaidia.

Alipelekwa kwenye zahanati ya wamishenali ilioko karibu na boma la mzee mambo usiku huo. Niliandama na wanakijiji wakoo wetu wenye wema walipmchukua mnuna wangu na kumpeleka hosipitalini.

Walipomfikisha walimwacha katika mikono ya nasi aliyekuwa kwenya zamu. Usiku huo ulikuwa mrefu sana kwangu kwani siku hiyo ndio nilisikia maneno mazito kutoka kwake aliponiambia kwa wizi ni mbaya na akaikata roho. Hiyo ndio siku usiku ambayo sitawaihi sahu